

# JARIDA LA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO



*Wizara ya Furaha*

Toleo Maalum la: 17 | 26 Juni, 2021 | [www.habari.go.tz](http://www.habari.go.tz)

## UMISSETA 2021 YAENDELEA KULETA HAMASA KUBWA



Wizara HabariTZ



Wizara\_habaritz



Wizara\_HabariTZ



**YALIYOJIRI KATIKA  
WA MASHINDANO YA  
MICHEZO YA UMISSETA  
26 Juni, 2021**

**KAULIMBIU: "MICHEZO SANAA NA  
TAALUMA KWA MAENDELEO YA  
UCHUMI WA VIWANDA"**

**NUKUU YA MRATIBU WA MPIRA WA  
KIKAPU NA KOCHA WA KIMATAIFA (FIBA)  
AGNES JOSEPH NJAVIKE**

**66**

Ninaipongeza Serikali kwa kufufua mashindano ya UMISSETA hapa nchini, mashindano haya yameleta hamasa kubwa.

Ninashauri mchezo wa Mpira wa Kikapu unzie kwenye ngazi za Shule za Msingi ili kuibua vipaji kuanzia ngazi chini.

Pia Maafisa Utamaduni wazingatie kuweka idadi sawa ya wachezaji wa kikapu kama inavyofanyika kwenye michezo mingine katika mashindano haya kwa kuwa mchezo wa kikapu ni mchezo unaokua hapa nchini.



**AGNES JOSEPH NJAVIKE**

**Mratibu wa Mpira wa Kikapu na  
Kocha wa Kimataifa (FIBA)**

# **UNGUJA WAIBUKA MABINGWA MCHEZO WA KURUSHA TUFE UMISSETA 2021**

Unguja na Shinyanga wameongoza kwenye mchezo wa kurusha Tufe katika Mashindano ya Taaluma na Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) kwenye fainali zilizofanyika leo Juni 26, 2021 mjini Mtwara.

Msemaji wa UMISSETA 2021, John Mapepele amesema Abdallah Salum kutoka Unguja ameibuka kuwa mshindi wa kwanza baada ya kurusha umbali wa mita 14 na sentimita 30 akifuatiwa na Edward Michaeli kutoka mkoa wa Dar es Salaam aliyerusha umbali wa mita 11 na sentimita 97 wakati nafasi ya tatu imechukuliwa na Rajabu Mtonyi kutoka Mkoa wa Dodoma aliyerusha umbali wa mita 11 na sentimita 47.

Kwa upande wa wasichana Keflonia Daudi kutoka Mkoa wa Shinyanga ndiye Mshindi wa kwanza kwa kurusha mita 8 na sentimita 93 akifuatiwa na Martha Matinga kutoka Simiyu aliyerusha umbali wa mita 8 na sentimita 88 ambapo nafasi ya tatu ilichukuliwa na Fatma Saidi kutoka Unguja aliyerusha umbali wa mita 8 na sentimita 70.

# MCHEZAJI BORA WA SIKU

MSHIRIKI ADAM MAKEME FAKHI KUTOKA UNGUJA NDIO  
MCHEZAJI BORA WA SIKU KWENYE MPIRA WA WAVU KWA  
WAVULANA.





66

Ninamshukuru na kumpongeza Rais wangu kwa kunifanya nishiriki mashindano haya ya UMISSETA 2021. Nimeongeza maarifa na marafiki kutoka mikoa mbalimbali ya nchi yetu ya Tanzania.

Mwaka 2018 nikiwa na umri wa miaka 13, Kocha wangu alinileta katika mashindano haya kama mtazamaji kwa kuwa aliona kipaji changu.

Nilimuahidi kupambana ili nije katika mashindano haya kama mchezaji. Namshukuru Mungu safari hii nimekuja kucheza na nimekuwa mionganini mwa wachezaji bora.

## **ADAM MAKAME FAKHI**

**Mchezaji mwenye uwezo wa kucheza nafasi nyingi katika mpira wa WavuShule ya Sekondari Jang'ombe - Unguja**

**MASHINDANO YA RIADHA  
MBIO MITA 3000 – WAVULANA**



# **MASHINDANO YA RIADHA MBIO MITA 3000 – WASICHANA**



# **MASHINDANO YA RIADHA KURUSHA TUFE – WASICHANA**

**MSHINDI WA KWANZA WA RIADHA YA KURUSHA TUFE KWA  
WASICHANA NI KEFLONIA DAUDI KUTOKA SHINYANGA,  
AMERUSHA UMBALI WA MITA 8 NA SENTIMITA 93.**



# **MASHINDANO YA RIADHA KURUSHA TUFU – WAVULANA**

**MSHINDI WA KWANZA RIADHA YA KURUSHA TUFU KWA  
WAVULANA NI ABDALLAH SALUM KUTOKA UNGUJA,  
AMERUSHA UMBALI WA MITA 14 NA SENTIMITA 30.**



# **MPIRA WA WAVU WASICHANA**

**MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA WAVU KWA  
WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 26, 2021. TIMU ZA  
MIKOA YA IRINGA 1 (WENYE BLUU) NA SINGIDA 3 (WENYE  
BLUU NYEUSI).**



# MPIRA WA WAVU WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA WAVU KWA  
WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 26, 2021. TIMU ZA  
MIKOA YA TANGA 3 (WENYE NJANO) NA SONGWE 0  
(WENYE NYEUSI).



# **MPIRA WA WAVU WAVULANA**

**MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA WAVU KWA  
WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 26, 2021. TIMU ZA  
MIKOA YA TABORA 1 (WENYE BLUU) NA SHINYANGA 3  
(WENYE NJANO).**



# **MPIRA WA KIKAPU WAVULANA**

**MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA KIKAPU KWA  
WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 26, 2021. TIMU ZA  
MIKOA YA ARUSHA 43 (WENYE NYEKUNDU) NA  
SINGIDA 9 (WENYE BLUU NYEUSI).**



# **SANAA ZA NDANI KWAYA**

**MASHINDANO YA UMISSETA UPANDE WA SANAA ZA NDANI  
(KWAYA) YAMEISHA LEO, JUNI 26, 2021. MIKOA  
ILIYOSHIRIKI LEO NI GEITA, IRINGA, RUKWA, TANGA,  
KILIMANJARO NA KIGOMA.**



**GEITA**



**IRINGA**



RUKWA



TANGA



KILIMANJARO



KIGOMA

# UMITASHUMTA | UMISSETA 2021



**#MwakaWavipaji**

**Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo  
S.L.P 25, 40470 DODOMA, TANZANIA**